

GOVERNMENT NOTICE No. 217 Published On. 26/2/2021

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

KANUNI

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 37A (4))

KANUNI ZA UTOAJI NA USIMAMIZI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE,
VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (MAREKEBISHO) ZA MWAKA 2021

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu (Marekebisha) za Mwaka 2021 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2019 ambazo katika Kanuni hizi zitajulikana kama “Kanuni Kuu”.

Tangazo la
Serikali
Na. 286 la
Mwaka 2019

Marekebisha ya
kanuni ya 3

2. Kanuni ya 3 ya Kanuni Kuu inafanyiwa marekebisha kwa kuweka tafsiri ya neno “mkopo” katika mpangilio wa kiherufi kama ifuatavyo:
“mkopo” maana yake ni mkopo wa fedha unaotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Kanuni hizi na ni pamoja na vifaa;”

Marekebisha ya
kanuni ya 6

3. Kanuni ya 6 ya Kanuni Kuu inafanyiwa marekebisha kwa kufuta aya (c) ya kifungu kidogo cha (1) na badala yake kuweka aya ifuatayo:
“(c) kikundi cha wanawake au vijana kina idadi ya wanakikundi wasiopungua watano na kwa kikundi cha watu wenye ulemavu, kina idadi ya wanakikundi wasiopungua wawili.”

Nyongeza ya
kanuni ya 6A

4. Kanuni Kuu zinafanyiwa marekebisha kwa kuongeza kanuni mpya ya 6A mara baada ya Kanuni ya 6 kama ifuatavyo:
“Mikopo 6A.-(1) Bila kujali masharti ya kanuni ya

kwa watu
wenye
ulemavu

6, mtu mwenye ulemavu atakuwa na sifa
ya kupata mkopo kama kikundi cha watu
wenye ulemavu endapo:

- (a) Kamati ya Kudumu ya Fedha, Mipango na Uongozi itajiridhisha kuwa mtu huyo amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu na sifa ya kuwa mwanakikundi wa kikundi cha watu wenye ulemavu;
 - (b) anajishughulisha na ujasiriamali au anakusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati;
 - (c) ana akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina lake kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali;
 - (d) ni raia wa Tanzania mwenye akili timamu na umri wa miaka kumi na nane na kuendelea;
 - (e) hana ajira rasmi.
- (2) Mtu mwenye ulemavu anayekusudia kuomba mkopo chini ya masharti ya kanuni hii atatakiwa kujaza fomu ya maombi ya mkopo itakayoambatishwa na nyaraka zifuatazo:
- (a) nakala ya cheti cha kuzaliwa au hati ya kiapo inayothibitisha kuzaliwa kwake;
 - (b) nakala ya leseni ya biashara au kitambulisho cha ujasiriamali kilichotolewa na Serikali;

- (c) nakala halisi ya taarifa ya akaunti kutoka katika benki ambayo ana akaunti;
- (d) nakala halisi ya barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa kwa kadri itakavyokuwa na Mtendaji wa Kata;
- (e) wazo la biashara.
- (3) Masharti mengine ya Kanuni hizi yatatumika kwa mtu mwenye ulemavu atakayepatiwa mkopo kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1)."

Marekebisho ya
kanuni ya 7

5. Kanuni ya 7 ya Kanuni Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kipengele cha (iii) cha aya ya (a) ya kanuni ndogo ya (3) na badala yake kuweka kipengele kifuatacho:

"(iii) kwa vikundi vinavyojishughulisha na biashara, leseni ya biashara ya kikundi au vitambulisho vya ujasiriamali vya wanakikundi vilivyotolewa na Serikali."

Marekebisho ya
kanuni ya 14

6. Kanuni ya 14 ya Kanuni Kuu inafanyiwa marekebisho kwa:

(a) kuingiza aya mpya ya (f) baada ya aya ya (e) katika kanuni ndogo ya (1) kama ifuatavyo:

"(f) Afisa Vijana wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na"; na

(a) kuibadili aya (f) kuwa aya (g).

Kufutwa na
kuwekwa upya
kanuni ya 23

7. Kanuni Kuu zinafanyiwa marekebisho kwa kufuta na kuweka upya Kanuni ya 23 kama ifuatavyo:

"Mafunzo
na
ufuatiliaji

23.-(1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakuwa na wajibu wa:

(a) kutoa mafunzo kwa vikundi

vilivyokubaliwa kupata mkopo katika masuala ya uongozi, usimamizi wa fedha, uendeshaaji wa miradi na utoaji wa taarifa hususan zinazohusu mkopo husika; na

- (b) kufanya ufuatiliaji wa mikopo na tathmini ya maendeleo ya vikundi vilivyopata mikopo.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka za Serikali za Mitaa zitatenga fedha kutoka katika fedha za marejesho ya mikopo kutoka kwenye vikundi kwa uwiano ufuatao:

- (a) Halmashauri yenye mapato ya ndani chini ya shilingi bilioni moja, itatenga shilingi laki tano hadi milioni moja kwa mwezi;

- (b) Halmashauri yenye mapato ya ndani ya shilingi bilioni moja hadi shilingi bilioni mbili, itatenga shilingi milioni moja hadi shilingi milioni moja na laki tano kwa mwezi;
- (c) Halmashauri yenye mapato ya ndani ya shilingi bilioni mbili hadi shilingi bilioni tano, itatenga shilingi milioni moja na laki tano hadi shilingi milioni mbili kwa mwezi; na
- (d) Halmashauri yenye mapato ya ndani ya shilingi bilioni tano na zaidi, itatenga shilingi milioni mbili hadi shilingi milioni tano kwa mwezi.”



Dodoma,
1 Februari, 2021

NAKUBALI,

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi